TANGAZO LA SERIKALI NA. 248 la tarehe 24/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA KINANAMBO YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itaitwa Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Kinanambo ya mwaka 2023.

Utangulizi wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (Mpango wa Urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la Kwenye Jedwali.

3. Mipangokina katika eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi wa Mji wa Mafinga.

*Tangazo la Serikali Na. 248 (Linaendelea.)*

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Mipango ya eneo itafanyika ndani ya mipaka ifuatayo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KNM 01 yenye majira – nukta 752217MS, 9082632KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.09 hadi unapokutana na barabara kuu ya TANZAM kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KNM 02 yenye majira – nukta 754360MS, 9084780KZ; baada ya hapo mpaka unafuata barabara kuu ya TANZAM kwa upande wa Kaskazini kwa umbali wa kilomita 0.45 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KNM 03 yenye majira – nukta 754485MS, 9085216KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki kwa kufuata barabara kuu ya TANZAM hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KNM 04 yenye majira – nukta 754526MS, 9085343KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.39 hadi unapokutana na barabara ya zamani ya Dar es Salaam kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KNM 05 yenye majira - nukta 754210MS, 9085571KZ; baada ya hapo mpaka unafuata
barabara ya zamani ya Dar es Salaam kwa umbali wa kilomita 0.49 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KNM 06 yenye majira – nukta 754165MS, 9085084KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KNM 07 yenye majira - nukta 754198MS, 9085063KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa umbali wa kilomita 0.23 hadi unapokutana na barabara ya zamani ya Dar es Salaam kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KNM 08 yenye majira – nukta 754184MS, 9084835KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KNM 09 yenye majira – nukta 754207MS, 9084817KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KNM 01 hadi ulipoanzia''

Dodoma,
6 Februari, 2023

BANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*